# KUKUMBUKA KAZI KUBWA ALIYOIFANYA YESU KRISTO MSALABANI KUNAUA KABISA ROHO ZOTE ZA KUKUKATISHA TAMAA KATIKA MAISHA YAKO.

## MAANDIKO: 1KOR. 11: 23- 26. (LUK. 22: 14 – 19)

1. **Kushiriki meza ya Bwana kusudi lake kubwa ni kutukumbusha gharama kubwa aliyolipa Bwana Yesu pale Msalabani ili sisi tupate wokovu, kuponywa magonjwa yote na kuinuliwa toka hali ya umaskini wa kutupwa na kuwa matajiri**. ***1Petro 2: 21-25, 2Kor. 8:9***
2. Hii ni siri ambayo hata nchi karibu zote zinafuata ya kukumbuka **siku ya uhuru wao, siku ya kutotawaliwa tena na Wakoloni, siku waliyopandisha bendera yao na kuishusha ile ya kikoloni!! Bila kukumbuka**, watu wanaweza kukata tamaa kutokana na mambo magumu wanayokutana nayo na kutamani watawaliwe tena na Wakoloni kama ambavyo wana wa Israel walipokutana na mambo magumu walikata tamaa na kutamani kutawaliwa na Farao aliyewatesa na kuwatumikisha mno. ***Kut. 14: 10 – 14, (Kut. 2: 23 - 25) – Siku zote akikutana na changamoto, kama hutakumbuka matendo makuu ya Mungu ni rahisi kabisa kusahau wema wote wa Yesu kwako.***

- Unajua, kuna wakati mteule anaweza kujikuta anapitia katika misukosuko kiasi cha kuchanganyikiwa na kushindwa kuelewa tena kwamba Mungu anamwazia mema na anayo mipango ya Baraka kwa ajili yake; Yesu anawataka wanafunzi wake wakumbuke aliyoyapitia yeye kwanza kama mwana wa Mungu kipenzi, walinganishe na wanayoyapitia wao kwanza na wakiona ya kwao ni madogo sana ukilinganisha na aliyoyapitia Bwana Yesu; wasonge mbele bila kukata tamaa kabisa.

“***Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana Yesu hata ajapo. 1Kor. 11: 26. Maana yake hasa ya mstari huu ni kwamba kila anayekula mkate (mwili wa Yesu) na kukinywea kikombe (divai) - damu ya Yesu Kristo) anatangaza wazi kwamba sasa anakuwa tayari kupokea faida zote zilizotokana na kifo cha Yesu Kristo pale Msalabani!!! Meza ya Bwana siyo swala la kidhehebu, ni maagizo maalumu kutoka kwa Bwana; na ikifanyika na watu walio na moyo safi, matokeo yake ni makubwa mno.***

***Note:*** **Kifo cha Yesu Kristo Msalabani na baadaye kuzikwana siku ya tatu akafufuka; ndiyo siri pekee ya imani hii tuliyonayo ambayo inashinda imani nyingine zote duniani pamoja na waanzilishi wake.** ***1Kor. 1: 18***

**3. <u>Yako maeneo makubwa matatu ambayo shetani anajitahidi sana kutukatisha tamaa na hasa akilenga kutufarakanisha na Bwana Yesu kwa kutaka tuone kwamba kifo chake pale Msalabani siyo chochote na ahadi zake zote kwetu siyo kweli. 2Kor. 1:20.</u>**

a. **Kitu cha kwanza anachokitumia sana na ambacho kinaongoza kwa watu wengi waliookoka vizuri na baadaye kukata tamaa kabisa na kuiacha imani hii takatifu ni MAZINGIRA.** ***Hes. 21: 1 – 9***

- Mazingira tunayokutana nayo yanaweza kabisa kutukatisha tamaa (**mfano wa binti yangu Mariamu na masomo yake),** mfano mwingine hai ni wa Yona aliyeitwa na Mungu kwenda Ninawi kupiga kelele (kuhubiri injili) Yona – **“HUA”**
- Kwa nini Wana wa Israeli walikufa moyo baada ya kufika katika Mji wa Ebroni!! wenyeji wa Mji huu waliwazuia wasipitie njia hiyo (Wamoabi) na kulazimika kurudi nyuma ili wazungukie Kadeshi njia ndefu mno wakati

walishabakiza mwendo wa siku mbili tu kuingia Yerusalemu- mazingira ya jinsi hii yanaweza kumfanya mtu kukata tamaa na kufa moyo kabisa- Mfano wa mama anayebeba mimba na kufika labour anazaa mtoto amekufa mara ya kwanza, ya pili, bila kukumbuka kwamba Yesu alipitia mateso magumu sana kabla ya kukirimiwa Jina lipitalo majina yote, lazima mazingira kama haya yatamvunja moyo!! ***Filip 2:5-11.***

b. **Jambo la pili ambalo shetani analitumia sana na ambalo kwa sasa nalielewa sawa sawa baada ya kuwa Kiongozi wa juu wa Kanisa letu *zuri* la EAGT ni TAARIFA *zinazomwijia* mwana wa Mungu. 2Wafal 20:1-6, Hesab 13:17-33, 14:1-10.** Kwa kweli kama Mfalme Hezekia asingekumbuka kumkumbusha Mungu utumishi wote aliotumika kwa ajili ya Mungu, taarifa aliyoletewa na Nabii Isaya ilikuwa ni ya kumuuwa kabisa!! Na kama taarifa mbaya ilivyowafanya wana wa Israel walie usiku kucha na kuasi kabisa, ndivyo hata leo kama taarifa hata zisizofaa ukiziruhusu au kufanya mjadala nazo kwenye ufahamu wako (mawazo), elewa umekwisha; shetani katika eneo hili la kuleta taarifa ni bingwa na taarifa zake anazileta akiwa amezichanganya na nusu ukweli na nusu uongo!! ***Mwanz 3:1-5, Neh 6:10-13*** yaani kwa kutumia akili zako kamwe huwezi kumshinda shetani.

- Zilitumwa taarifa nyingi mno wakati Yesu Kristo alipokuwa amepigiliwa msalabani!! ***Luk 23:35, Mt 27:45-46*** na Yesu hakujibu kila taarifa, alichuja kabla ya kujibu.
- Chuja taarifa, siyo lazima ujibu kila taarifa au swali, taarifa nyingine nyamaza!! ***Mark 14:55-65***

***c.*** **Jambo la tatu kubwa na hatari zaidi ambalo shetani analitumia na ambalo hata mimi mwenyewe nina ushahidi nalo ni shetani kutumia watu wa karibu**

**sana na wewe- (marafiki).** ***Zab. 55:12-14, Ayub 2:9-10, 42:7-9*** shetani kamwe hatatumia watu walio nje kukukatisha tamaa katika safari hii, atatumia walio karibu sana na wewe kama alivyomtumia Yuda kumsaliti Yesu. ***Mark 14:10-11***

- Waliojaribu kumkatisha tamaa Mtume Paulo ni wale watumishi wenzie tena kwa kutoa unabii!! ***Mdo 21:8-14, Neh. 6:10-13*** na hata waliojaribu kumkatisha kabisa tamaa ya kwenda kupigana na Goliath ndugu yetu Daudi ni ndugu zake pamoja na boss wake Mfalme Sauli!! ***1Sam 17:28-37***, **ukikumbuka kwamba Yuda alijutia ujanja wake baadae, hutawaogopa wanaokusaliti leo maana kesho yatawageuka.** ***Zab 30:11***

4. Kula mwili wa Bwana Yesu leo na kunywa damu yake, kutupatie kumbukumbu kwa upya kwamba Yesu Kristo alimaliza yooote pale msalabani, na hata hilo linalojaribu kufurukuta mbele yetu lilikwisha shindwa miaka zaidi ya **2000** iliyopita pale msalabani.

- Leo ni siku ya **kutangaza** na kupokea faida za kifo cha Bwana Yesu msalabani. ***1Kor 11:26***
- Faida za msalabani ni nyingi zikiwemo za **wokovu, uponyaji wa magonjwa, kufunguliwa toka hali ya umaskini wa kutupwa na kufanywa matajiri , kulindwa na nguvu ya Mungu; kupewa mamlaka ya kutawala, kuishi kama Wafalme hapa duniani** n.k Lazima tukumbuke kwamba bila Yesu Kristo kulipa gharama zote, sisi tusingefurukuta mbele ya Ulimwengu huu, lakini sasa tunashinda na zaidi ya kushinda. ***1Yoh 5:4-5*** . **Amina**

***Na.***

***Ask.Dr L. Mwizarubi***
***Sept 2021***